# Msaada juu ya ukeketaji

By SW - Melkisedeck Shine · April 16, 2022

Ujana na Makuzi | Mapenzi na Ngono Salama

Unaweza ukajaribu kuzungumza na wazazi wako kwamba ukeketaji ni desturi mbaya, na pia unaweza ukamtafuta mtu wa kukusaidia ambaye ni mwaminifu. Msaidizi anaweza akawa rafiki, mlezi, mzazi au mtu mzima katika familia ambaye unaweza kumwamini. Katika jamii yako unaweza kumtafuta mwalimu anayeaminika, kiongozi wa dini au muuguzi ambaye anaunga mkono mawazo yako na mwenye msimamo wa kumaliza tatizo la ukeketaji.

Kama hakuna mashirika yanayopinga ukeketaji katika sehemu yako, unaweza kufikiria watu wanaofanya katika shirika la vijana, vituo vya vijana, jumuia za wanawake, makanisa na mashirika ya uzazi wa mpango. Unaweza kutoa habari hii katika kituo cha afya kilicho karibu nawe. Kumbuka vijana chini ya miaka 18 ukeketaji ni kosa la jinai na unaweza kuripoti katika kituo cha polisi kilicho karibu nawe.